

SHULE YA SEKONDARI MRAOKERYO

S.L.P 128-MKUU-ROMBO

SIMU +225755642415

+225787633872

KWA MZAZI/MLEZI WA.....

YAH: MAELEKEZO YA MWANAO KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MRAOKERYO
MWAKA 2021.

1:0 MADHUMUNI YA ELIMU

Kumpatia mwanafunzi elimu ujuzi, maarifa na maadili ambayo yatamuwezesha kuchukua nafasi yake katika kutumikia taifa lake na kumuwezesha kupata mapato halali kwa kazi atakayoifanya na dunia ya sasa yenye mabadiliko ya sayansi ,teknolojia na utandawazi.

1:1 MASOMO YATAKAYOFUNDISHWA

1:URAIA 2:KISWAHILI 3: KINGEREZA 4: HISTORIA 5: BIOLOJIA

6: HISABATI 7: FIZIKIA 8:KEMIA 9:JIOGRAFIA 10: FASIHI YA KINGEREZA 12: DINI

Kwahiyo mwanao aje na madaftari makubwa (3Quires) yasiopungua kumi na moja na pia anunue madaftali mengine kumi madogo yakufanyia mazoezi mbalimbali (weekly test).

1:2 MALIPO YA SHULE

Gharama ya chakula na michango mingine ya shule itaamuliwa katika kikao cha wazazi kitakachofanyika Januari, 2021

NB: Gharama hizi hazihusiani na matibabu ya mtoto pindi anapougua akiwa shuleni kwani shule inatoa huduma ya kwanza tu, jukumu la kumpeleka hospitali ni la mzazi.

1:3 SARE RASMI YA SHULE

Wanafunzi wote wanatakiwa wawe na sare rasmi ya shule kama ifuatavyo:

1:3:1 WAVULANA

(a) Suruali ndefu mbili (02) za rangi ya brauni

(b) Shati nyeupe mbili (02) kitambaa tetroni (linalong'aa) lenye mikono mifupi .

(c)Viatu vya ngozi vyeusi vyenye kamba na visivyopiga kelele sakafuni na visiwe na visigino virefu

(d) Tai ndefu ya blauni yenye mistari rangi nyeupe

(e) Sweta la rangi brauni lenye mistari miwili rangi nyeupe kifuani.

(f) Aje na shilingi 10000/- kwaajili ya Tshirt

1:3:2 :WASICHANA

(a) Sketi ndefu mbili (02) za rangi ya brauni(kahawia)

(b) Shati (blauzi) nyeupe mbili (02) kitambaa tetroni (linalong'aa) lenye mikono mirefu lenye vifungo vya kushonea na sio vya chuma.

I Tai ndefu ya brauni yenye mistari rangi nyeupe

(d) Viatu vya ngozi vyeusi vyenye kamba na visivyopiga kelele sakafuni na visiwe na visigino virefu pairs mbili (02)

I Sweta la rangi brauni lenye mstari mweupe kifuani,

(f) Aje na shilingi 10000/- kwaajili ya Tshirt

NB: Sare ziwe mpya

Ni vyema mzazi/mlezi ukamuandalia mapema mwanao mahitaji hayo ya shule.

VIFAA VINGINE MUHIMU:

Mwanao anapokuja shuleni aje na:

(i) Mkebe wa vifaa vya mahesabu(compass)

(ii) Sahani na bakuli ya kulia chakula

(iii) Begi la Vitabu, Daftari na vifaa vyake vingine.

(iv) Kamusi ya Kingereza (Dictionary)

(v) Rimu 01

(vi) Ndoo ndogo na fagio la chelewa

N.B:

SHULE ITAFUNGULIWA TAREHE 11/01/2021 HIVYO MZAZI/MLEZI UMLETE MWANAO SAA 01:30 ASUBUHI AKIWA NA MAHITAJI YOTE PAMOJA VIFAA VYOTE VINAVYO HITAJIKA KWAAJILI YA KUANZA MASOMO NA KIKAO CHA WAZAZI KITAFANYIKA TAREHE 21/01/2021, HIVYO UKIWA KAMA MZAZI AU MLEZI UNAOMBWA KUPIKA SIKU HIYO BILA KUKOSA ILI KUJADILI MAENDELEO YA SHULE YETU.

**“KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI
MRAOKERYO KWA ELIMU BORA NA YENYE
MANUFAA”**

FORM A

PRESIDENT’S OFFICE

REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT(PM0-RALG)

MRAOKERYO SECONDARY SCHOOL

MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by Medical officer in Government Hospital in respect of all new entrants to Mraokeryo Secondary School.

Full name.....

Age.....

1.'AIDS' test.....

2.Blood Count (Red & White).....

3.Stool examination.....

4.Urine examination.....

5.Syphils.....

6.T.B. Test.....

7.Eye Test.....

8.Ear Test.....

9.Speech.....

10.Abdomen.....

11.Additional information or any physical, mental, heredity
infection/disease.....

.....

Treatment after examination (Please state nature of treatment)
.....

Medical Certificate

I certify that above mentioned has been examined and found fit/unfit to pursue future education.

Signature.....

Designation.....

FOMU B

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

SHULE YA SEKONDARI MRAOKERYO

FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2020

Fomu hii ijazwe na mzazi/mlezi pamoja na mwanafunzi aliyechaguliwa kidato cha kwanza kasha mwanafunzi ailete shuleni (Ithibitishwe na Afisa Mtendaji wa Kata yake)

1.Mimi.....(Mwanafunzi) kwa hiari yangu mwenyewe ninakubali/Sikubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Mraokeryo. Nitakuwa tayari kuzifuata sheria zote za shule wakati wote niwapo Shuleni, kuvunja sheria za shule makusudi nitakuwa nimekimekiuka ahadi ninayotoa na ninastahili kuchukuliwa hatua za kinidhamu.

Sahihi ya mwanafunzi.....

Tarehe.....

2.Mimi.....(Mzazi/Mlezi) Naikubali/Siikubali nafasi aliyopewa motto wangu na kwamba muda wote awapo shuleni analazimika kufuata sheria za shule na kuwa mtii kwa walezi wake. Pia nikiwa kama Mzazi/mlezi wake naahidi kushikiana na uongozi wa shule katika malezi yote na kwamba nitamlipia gharama zote zitakazomwezesha kusoma bila pingamizi wala kisingizio chochote.

Sahihi ya Mzazi/Mlezi.....

Tarehe.....

3.Mimi.....nathibitisha kuwa ndugu.....

ni Mzazi/Mlezi wa motto aliyechaguliwa kuingia kidato cha kwanza shule ya Sekondari Mraokeryo.

Nimeshauriana nae kuhusu wajibu wa mwanae na amekiri kutimiza wajibu wake ipasavyo.

Sahihi ya Afisa Mtendaji.....

Kata ya

FOMU C

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

SHULE YA SEKONDARI MRAOKERYO

FOMU YA KUJIANDIKISHA SHULENI: SEHEMU YA HABARI YA MZAZI/MLEZI

1.Jina kamili.....

- 2.Kazi yake.....
- 3.Nyumbani kwake.....
- 4.Anuani ya nyumbani.....Kijiji.....Kata.....
Tarafa.....Wilaya.....Mkoa.....
- A:Anuani ya mahari pakazi Mzazi/Mlezi.....
- B: Nambari za simu 1: 2:.....
- 5:Dini ya Mzazi/Mlezi
- 6:Dhebu unalotaka mwanao alelewe awapo shuleni.....
- 7.Anuani kamili ya nyumbani ambako motto atakwenda siku za likizo.....
.....
- 8.Anuani ya Kazini (Ikiwa inatofautiana na hiyo hapo juu) kila mara inapobadilika tunaomba utuarifu rasmi kwa mkuu wako wa kituo au kijiji chako.....
- Ninaahidi kushirikiana na walimu na watumishi ili kuhakikisha kwamba kijana/binti yangu anakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi na mwenye bidii katika masomo.
- MimiMzazi/Mlezi nanathibitisha kuwa maelezo hayo hapo juu ni sahihi.
- Tarehe.....
- Sahihi.....

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu . Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

- (a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- (b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- (c) Kuwahi katika kila shughuli ya shule na nyingine utakazopewa.
- (d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- (e) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- (f) Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa.
- (g) Kutunza mali za umma.

MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

- (a) Wizi
- (b) Uasherati na Ushoga
- (c) Ubakaji
- (d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyo kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kuberi na kadhalika.
- (e) Kupigana au Kupiga
- (f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- (g) Kudharau Bendera ya Taifa
- (h) Kuwa mjamzito/kupata mimba
- (i) Kutoa mimba
- (j) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani ya na usalama wa shule au watu
- (k) Kukataa adhabu kwa makusudi
- (l) Kuwa na simu ya mkononi

MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI

(a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya serikali , Fomu hii itakabidhiwa kwa Makamu Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.

(b) Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo,fujo na makosa ya jinai .

(c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria ,kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

N.B:

*MZAZI/MLEZI AHAKIKISHE ANAMPELEKA MTOTO HOSPITALI YOYOTE YA SERIKALI KWAAJILI YA KUFANYIWA VIPIMO VYA AFYA KISHA **AJE NA RISITI YA MALIPO** YA HOSPITALI KUTHIBITISHA AMEFANYIWA VIPIMO.*